# Kifurushi cha Orodha ya Matayarisho ya Masomo ya Kabla ya Chekechea/Shule ya Chekechea

## 1. Mwanafunzi anaitikia kwa kukubali anapotenganishwa na m(wa)zazi.

*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za kitabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha

Lengo ni kutambua iwapo mwanafunzi anaweza kuwa peke yake mbali na wazazi.

a. Waulize wazazi maoni yao ikiwa wanaamini kuwa mtoto wao anaitikia kwa kukubali anapotenganishwa nao.
b. Wape fursa jamaa wote (isipokuwa mwanafunzi) wasimame na watembee kuenda eneo lingine (ambapo mwanafunzi hawezi kuwaona). Au ujaribu kumchukua mwanafunzi na kuenda naye kwenye sehemu nyingine (ambapo mwanafunzi hawezi kuwaona).
c. Ikihitajika mshughulishe mwanafunzi-kuwa mcheshi, fanya mzaha, ili mtoto avutiwe nawe. Muulize mwanafunzi ataje jina lake? Muulize mwanafunzi ana umri gani?
d. Ona jinsi mwanafunzi anavyoitikia.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **ALAMA** | ☐ **Bado**<br>Ana tatizo la kutengana (analia, anakataa kuenda au anasalia, anaonyesha hasira nyingi). | ☐ **Anaendelea Kujua**<br>Huenda akaona haya au analia kwa muda mfupi tu. | ☐ **Ndiyo**<br>Anatengana kwa urahisi na kwa furaha. | ☐ **Haitumiki**<br>Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa. |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi anaanza kulia.<br>Mwanafunzi anaanza kukimbia akiifuata familia yake.<br>Mwanafunzi anakataa kujibu swali lolote. | **Mifano**<br>Mwanafunzi amekasirika lakini anamruhusu mtu mzima kumtuliza.<br>Mwanafunzi anajibu maswali. | **Mifano**<br>Mwanafunzi hadhihirishi mwitikio wowote kwa utengano.<br>Mwanafunzi ni mtulivu.<br>Mwanafunzi anajibu maswali. | **Mifano/Eleza**<br>Mwanafunzi hajawahi kamwe kutenganishwa na m(wa)zazi. |

## 2. Mwanafunzi anawatambua jamaa wa karibu na sifa zao.

*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha

*** Kiashirio hiki kinaungwa mkono na Kiambatisho cha E : Familia Yangu (Ukurasa wa 49).

Lengo ni kutambua "sifa" 3 za jamaa wao wa karibu.

- Jina la Kuzaliwa / Jina Rasmi / Jina la Utani (Victor, Jose, Maria, Brenda) – Jina la kwanza, la mwisho, la utani linatambuliwa.
- Uhusiano wa Familia (mama, baba, dada, kaka, mpwa, binamu, mjomba, shangazi, n.k.)
- Sifa Moja ya jamaa (umri, kazi, mambo yanayomvutia, chakula, kinywaji, au shughuli anayoipenda zaidi, n.k.) Mtoto anaweza kuhesabika kama mmoja wa jamaa.

a. Muulize mwanafunzi awatambue jamaa zake wa karibu. Ikiwa wako ndani ya chumba, mwambie mwanafunzi awaashirie na kutaja majina yao. Ikiwa kuna picha ya familia, itumie.
b. Jamaa wa karibu huzingatiwa kuwa ni: Mama, Baba, Dada, Kaka na m(wa)nyama k(v)ipenzi.
c. Hakikisha mwanafunzi anatambua kila jamaa kwa kutaja jina lake (jina rasmi na/au jina la utani; Victor, Jose, Maria, Brenda) na uhusiano wao wa familia (mama, baba, dada, n.k.)
d. Muulize mwanafunzi aseme jambo fulani analojua kumhusu kila jamaa (umri - kazi zao - mambo yanayowavutia, chakula au kinywaji au shughuli wanayopenda zaidi).

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **ALAMA** | ☐ **Bado**<br>Anataja kimoja kati ya vitambulisho vitatu vya jamaa. | ☐ **Anaendelea Kujua**<br>Anataja viwili kati ya vitambulisho vitatu vya jamaa. | ☐ **Ndiyo**<br>Anataja vitambulisho vyote vitatu vya jamaa. | ☐ **Haitumiki**<br>Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa |
| **MADOKEZO** | **Mifano** Mwanafunzi hawezi kuwatambua jamaa zake wa karibu.<br>Mwanafunzi anataja majina yasiyo sahihi. | **Mifano** Mwanafunzi anaweza kutambua m(wa)zazi wake na ndugu zake wa karibu lakini hawezi kujadili ulinganifu na tofauti kati yake mwenyewe na wengine. Mimi ni Victor, huyo ni dadangu. | **Mifano** Jina langu ni Ela na kakangu Jimmy hupenda malori, lakini mimi hupenda magari madogo.<br>Huyo ni babangu Cole, yeye ni mzee, na huyu ni paka wangu, Spot, anapenda maziwa. | **Mifano/Eleza:** |

### 3. Mwanafunzi anatambua mizozo rahisi na anajaribu kuitatua mwenyewe.

✧ *** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha.

◯ *** Kiashirio hiki huenda kikaripotiwa na familia.

☆ *** Kiashirio hiki kinaungwa mkono na Kiambatisho cha F: Mikakati ya Kusuluhisha Mizozo (ukurasa wa 50)

Lengo ni mwanafunzi aweze kusuluhisha mzozo na kuzingatia hitaji la wengine.

a. Ikiwezekana, mwangalie mwanafunzi anapotangamana na watoto wengine (au jamaa).
b. Ikiwa hilo haliwezekani iulize familia iripoti kuhusu kiashirio hiki.
c. Mzozo baina ya ndugu kwa kawaida huwa kuhusu chombo fulani.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **ALAMA** | ☐ **Bado**<br>Anapokumbwa na mzozo, anaeleza mahitaji na haja zake, lakini anahitaji usaidizi ili kutoa suluhu zinazowezekana. | ☐ **Anaendelea Kujua**<br>Anapendekeza suluhu rahisi za mzozo ambazo aghalabu zinazingatia mahitaji na haja zake mwenyewe. | ☐ **Ndiyo**<br>Anapendekeza suluhu za mzozo huku akizingatia mahitaji na haja zake na za wengine. | ☐ **Haitumiki**<br>Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi anatazama familia yake na kupiga kelele akiitisha kitabu chake.<br>Mwanafunzi anamtazama mtu mzima ili amsaidie kurudisha chombo chake.<br>Mwanafunzi anakasirika, anaanza kupigana au kuudhika. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anatumia maneno yake: "Ni zamu yangu ya kusoma kitabu hicho. Nipe utakapomaliza kukitumia."<br>Mwanafunzi anajaribu kubadilishana kitabu au kalamu na kifaa kingine alicho nacho.<br>"Unaweza kutumia hii penseli yangu ikiwa utaniruhusu nikitumie kwanza." | **Mifano**<br>Wanafunzi wanaomba watumie kifaa kwa dakika 5.<br>Mwanafunzi anaingilia kati wakati wengine wanapobishana na kuwatuliza.<br>Mwanafunzi anatumia maneno yake: "Ninahitaji kitabu hicho sana - tunaweza kukisoma pamoja? - tunaweza kupaka rangi pamoja?" | **Mifano/Eleza:** |

### 4. Mwanafunzi anatambua kanuni na anajadili sababu za kuwa na kanuni mahususi.

✧ *** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha.

◯ *** Kiashirio hiki huenda kikaripotiwa na familia.

Lengo ni mwanafunzi atambue hali zisizo salama na aweze kueleza kanuni mahususi na ni kwa nini ipo.

a. Wakati mtu mzima yupo, na mtoto anahusika na hali isiyo salama angalia mwitikio wa utekelezaji wa kanuni.
b. Ikiwezekana, angalia tabia hii mwanafunzi anapotangamana na wengine (watoto, jamaa, n.k.).
c. Ikiwa hilo haliwezekani iulize familia iripoti kuhusu kiashirio hiki.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **ALAMA** | ☐ **Bado**<br>Anapohitajika kufuata kanuni, hawezi kudhibiti mwitikio wake na analia, kukataa au kuonyesha hasira nyingi. | ☐ **Anaendelea Kujua**<br>Anapohitajika kufuata kanuni, anahitaji usaidizi wa kufuata kanuni. | ☐ **Ndiyo**<br>Anafuata kanuni ipasavyo na anaweza kueleza sababu za kuwepo kwa kanuni hizi. | ☐ **Haitumiki**<br>Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi anakimbia, na anapoambiwa atembee, anaendelea kukimbia au kuonyesha hisia.<br>Mwanafunzi anakataa kuvaa jaketi yake anapoenda nje kukiwa na baridi.<br>Mwanafunzi anajaribu mipaka iliyowekwa na watu wazima. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anapanda kwenye fanicha, na anapoambiwa ashuke akanyage chini kwa miguu 2, anashuka. Kisha dakika 10 baadaye anahitaji kukumbushwa kanuni hiyo hiyo.<br>Mwanafunzi anahitaji kukumbushwa na watu wazima afuate kanuni zao. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anawaambia wengine wasalie kando ya barabara na wasitembee kwenye barabara.<br>Mwanafunzi anakuambia ukalie kiti, ili usianguke.<br>Mwanafunzi anafuata kanuni na anaweza kueleza sababu ya kanuni hizo kwa wengine (ndugu). | **Mifano/Eleza:** |

## 5. Mwanafunzi anafahamu jina lake la kwanza, jina lake kamili na umri wake, na anaweza kuhusisha baadhi ya herufi na jina lake na sauti.

△ ☆

***Wanafunzi wa ELL/DLL wanapaswa kupewa alama ya weledi wao wa Kiingereza kwa kiashirio hiki.

*** Kiashirio hiki kinaungwa mkono na Kiambatisho cha G : Jina.

Lengo ni mwanafunzi aweze kutaja maelezo yake na kutambua angalau herufi 2 kati ya alfabeti ya Kiingereza.

a. Huku unapomuuliza maswali kwa Kiingereza na lugha yake asili (ikihitajika), nakili majibu yake kwenye karatasi kubwa nyeupe. Unaweza kumuuliza mwanafunzi kufanya hivyo - kuandika majibu yake kwenye karatasi kubwa tofauti nyeupe.
b. Muulize jina lako ni gani? Andika jina hilo. Jina la kwanza au la utani ni sahihi.
c. Jina lako la mwisho ni gani? Andika jina hilo. Jina la mwisho la mwanafunzi linaweza kuwa tofauti na lile la jamaa wale wengine.
d. Una umri gani? Andika nambari ya umri wa mwanafunzi.
e. Angalia karatasi yako (na yake) muulize mwanafunzi ataje herufi za jina lake na uthibitishe iwapo mwanafunzi anatambua na kutaja herufi mbili.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **ALAMA** | ☐ **Bado**<br>Anatambua kwa usahihi moja kati ya maelezo manne aliyoulizwa. | ☐ **Anaendelea Kujua**<br>Anatambua kwa usahihi mawili kati ya maelezo manne aliyoulizwa. | ☐ **Ndiyo**<br>Anatambua kwa usahihi maelezo manne kati ya manne aliyoulizwa, iwe ni kwa kujibu kwa kutumia maneno au bila kutumia maneno. | ☐ **Haitumiki**<br>Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi anataja jina sahihi la kwanza (na/au jina la utani), lakini jina la mwisho na umri si sahihi. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anataja jina sahihi la kwanza na anaashiria idadi sahihi ya vidole ili kuonyesha umri wake. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anataja jina sahihi la kwanza.<br>Mwanafunzi anataja jina sahihi la mwisho.<br>Mwanafunzi anatoa jibu sahihi la umri wake.<br>Mwanafunzi anatambua kwa kuona au kusema na kutaja angalau herufi mbili za jina lake. | **Mifano/Eleza:** |

## 6. Mwanafunzi anatofautisha herufi na nambari.

△ ☆

***Wanafunzi wa ELL/DLL wanapaswa kupewa alama ya weledi wao wa Kiingereza kwa kiashirio hiki.

*** Kiashirio hiki kinaungwa mkono na Kiambatisho cha H : Alfabeti na Kadi za Nambari.

Lengo ni mwanafunzi atofautishe NA kutaja baadhi ya herufi na nambari. Tumia kadi za alfabeti na nambari, zikiwa zimechanganyika.

a. Chukua kadi kutoka kwa rundo moja na umuulize mwanafunzi ikiwa hiyo ni herufi au ni nambari? Usihesabu majibu asiyo na uhakika nayo. Ninafikiri ni mbili - Je, ni mbili?
b. Kisha mwanafunzi anatengeneza marundo mawili (ukimsaidia). Moja la Herufi na Lingine la Nambari.
c. Muulize mwanafunzi ataje jina la kila herufi na/au nambari. Ikiwa mwanafunzi hajui, anaruhusiwa kutotambua herufi na nambari hizo.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **ALAMA** | ☐ **Bado**<br>Anatambua baadhi ya herufi AU baadhi ya nambari. | ☐ **Anaendelea Kujua**<br>Anatambua baadhi ya herufi na baadhi ya nambari, hata hivyo anataja tu majina ya baadhi ya herufi au nambari. | ☐ **Ndiyo**<br>Anatambua NA kutaja majina ya baadhi ya herufi na baadhi ya nambari. | ☐ **Haitumiki**<br>Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi anafanya makosa mengi katika kutofautisha herufi na nambari.<br>Mwanafunzi hawezi kutambua herufi au nambari kwa Kiingereza.<br>Mwanafunzi anatumia jina moja la nambari kutambua nambari kadhaa.<br>Mwanafunzi anaomba usaidizi: Ninafikiri ni nne? Je, ni tano? Je, ni a? | **Mifano**<br>Mwanafunzi anataja herufi au nambari kwa usahihi lakini anaiambatanisha na kadi tofauti.<br>Mwanafunzi anatambua herufi "H" na anasema jina langu linaanza na "H" na kutaja sauti ya H lakini anaweka kadi hiyo kwa rundo la nambari. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anaweka kadi zenye 0, 2, 3, 1 kwenye rundo linalofaa na anasoma nambari kwa usahihi kwa Kiingereza.<br>Mwanafunzi anasoma herufi, a, b, c, d, e, f, h, k na p na kutambua kuwa ni herufi. | **Mifano/Eleza:** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **7. Mwanafunzi anatambua jalada la mbele, jalada la nyuma na kichwa cha kitabu - Anadhihirisha ufahamu wa muundo wa matini.**<br>*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha.<br>*** Kiashirio hiki huenda kikaripotiwa na familia.<br>*** Kiashirio hiki kinaungwa mkono na Kiambatisho cha I: Sehemu za Kitabu. | | | | |
| Lengo ni mwanafunzi kutambua mwelekeo sahihi wa kitabu, jalada la mbele na la nyumba la kitabu.<br>a. Mwambie mwanafunzi achukue kitabu au atumie kitabu ambacho umechukua. Sema, "Leo tutasoma kitabu pamoja."<br>b. Mpe mwanafunzi kitabu kikiwa kimepinduliwa juu chini na kikionyesha sehemu ya nyuma. Ona jinsi mwanafunzi anavyoitikia.<br>c. Muulize mwanafunzi asome kitabu na uangalie ikiwa mwanafunzi anafuatilia maneno kutoka upande wa kushoto hadi wa kulia.<br>d. Tumia kitabu hicho kumuuliza mwanafunzi kuhusu pale jalada la mbele, jalada la nyuma, na kichwa kilipo.<br>e. Muulize mwanafunzi akuambie kile anachokiona. | | | | |
| **ALAMA** | ☐ **Bado**<br>Haonyeshi kuvutiwa na kitabu. | ☐ **Anaendelea Kujua**<br>Anatumia ujuzi wa kuanzia wa kushughulikia kitabu. | ☐ **Ndiyo**<br>Anatumia sehemu za kitabu (kichwa, jalada la mbele, jalada la nyuma) ili kuyafahamu maandishi. | ☐ **Haitumiki**<br>Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi anashika kitabu sehemu ya juu ikiwa chini.<br>Mwanafunzi hajifanyi anasoma kitabu.<br>Mwanafunzi anatambua maandishi anayofahamu anapoambiwa kichwa cha kitabu. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anaweza kutambua jalada la mbele, na jalada la nyuma, lakini haonyeshi ufahamu wa muundo wa matini.<br>Mwanafunzi anashika kitabu kwa mwelekeo unaofaa lakini hashughuliki na kufuatilia maneno.<br>Mwanafunzi anaashiria maneno, kutoka kushoto hadi kulia, huku akijifanya anasoma hadithi. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anasema, "Tazama, nina paka pia", anapoashiria jalada la mbele ambalo linaonyesha paka.<br>Mwanafunzi anatumia michoro iliyoko kwenye kitabu ili kumsimulia rafiki yake hadithi anayoijua. | **Mifano/Eleza:** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **8. Mwanafunzi anasimulia mfululizo rahisi wa matukio kwa kutumia picha.**<br>*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha.<br>*** Kiashirio hiki kinaungwa mkono na Kiambatisho cha J : Kadi za Picha za Mfululizo. | | | | |
| Lengo ni mwanafunzi atambue mfululizo sahihi anapozitazama picha.<br>a. Tumia viambatisho vya karatasi za mazoezi ya mfululizo vilivyopeanwa.<br>b. Mwelezee mwanafunzi kwamba ni lazima afafanue ni nini kilichoendelea kwanza.<br>c. Ikiwa mwanafunzi anasita na anaomba usaidizi, mnaweza kufanya mfano 1 pamoja. Tumia mfano wa paka aliyeenda kuogelea.<br>d. Ikiwa mwanafunzi bado anatatizika, unaweza kumwelezea mfano ule ule tena. Usimpe vidokezo, mapendekezo au uthibitisho wa kile ambacho ni kizuri au si kizuri.<br>e. Mpe mwanafunzi jumla ya dakika 5 kufanya zoezi hili. Huenda wakabadilisha mfululizo wa matukio hadi dakika 5 ziishe. Wakati huo ndio utakapohesabu mifululizo sahihi ya matukio. | | | | |
| **ALAMA** | ☐ **Bado**<br>Anafanya mifululizo 4 au chache sahihi. | ☐ **Anaendelea Kujua**<br>Anafanya kati ya mifululizo 5 au 8 sahihi. | ☐ **Ndiyo**<br>Anafanya mifululizo 9 au zaidi sahihi. | ☐ **Haitumiki**<br>Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi haelewi cha kufanya (hata kwa lugha yake kuu).<br>Mwanafunzi anatoa maelezo kuhusu picha lakini hawezi kuzipanga kwa mfululizo sahihi. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anaweza kukamilisha mifululizo 5, 6, 7, au 8 sahihi.<br>Mwanafunzi anasimulia hadithi kuhusu picha na anaweka baadhi ya picha hizo kwa mfululizo sahihi. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anaweza kukamilisha mifululizo 9, 10 au zaidi sahihi.<br>Mwanafunzi anasimulia hadithi kuhusu picha na anaweka picha hizo kwa mfululizo sahihi. | **Mifano/Eleza:** |

## 9. Mwanafunzi anaandika jina kwa kutumia miundo inayofanana na herufi au maandishi ya kawaida.

***Wanafunzi wa ELL/DLL wanapaswa kupewa alama ya weledi wao wa Kiingereza kwa kiashirio hiki.

Lengo la mwanafunzi ni kuonyesha kuwa anaweza kuandika jina lake.

a. Muhimize mwanafunzi aandike jina lake kwenye karatasi.
b. Mruhusu mwanafunzi achague kifaa cha kuandika nacho (kalamu ya kuandikia alama, penseli, n.k.) na umuhimize mwanafunzi kutaja herufi anapokuwa akiziandika.
c. Ikiwa inahitajika, unaweza kutumia kazi ya sanaa iliyotengenezwa hapo awali (yenye jina la mwanafunzi) na umuulize mwanafunzi akuonyeshe na akuambie kile ambacho aliandika/alichora.

| ALAMA | ☐ **Bado** | ☐ **Anaendelea Kujua** | ☐ **Ndiyo** | ☐ **Haitumiki** |
|---|---|---|---|---|
| | Anaandika sehemu za miundo ya herufi (k.m., mistari, vizingo). | Anaandika herufi au maumbo yanayofanana na herufi. | Anaandika jina lake na/au maneno rahisi, huku nyingi za herufi zikiwa sahihi. | Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa. |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi anachorachora mistari, miduara, mistari mshazari, au kwa safu-milalo. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anachora herufi.<br>  | **Mifano**<br><br> | **Mifano/Eleza:** |

## 10. Mwanafunzi anafuata maagizo anapopewa maelekezo ya hatua mbili.

*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha.

*** Kiashirio hiki kinaungwa mkono na Kiambatisho cha K: Mfululizo: Maelekezo yenye Hatua Nyingi.

Lengo ni mwanafunzi aweze kujibu bila usaidizi anapoulizwa swali linalohitaji kitendo cha hatua mbili.

a. Muulize mwanafunzi afanye hatua au agizo au kuanzisha hatua inayofuata kwenye mfululizo na kisha na umuhimize kuendelea anapopata matokeo yanayofaa.
b. Mpe mtoto fursa ya kurudia hatua hadi afahamu kila mojawapo vizuri.
c. Tumia kiambatisho cha K. kwa mifano mahususi.
d. Mpe mwanafunzi muda wa kujibu.

| ALAMA | ☐ **Bado** | ☐ **Anaendelea Kujua** | ☐ **Ndiyo** | ☐ **Haitumiki** |
|---|---|---|---|---|
| | Anafuata maelekezo yenye hatua moja au mbili anapokumbushwa. | Anafuata maelekezo yenye hatua moja au mbili. | Anajibu kauli rahisi na anaonyesha kuelewa dhamira. | Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi anaenda kwenye sinki kunawa mikono, lakini anahitaji usaidizi kufuata utaratibu unaofaa (kuweka sabuni, kufungulia maji, n.k.) | **Mifano**<br>Mwanafunzi anatupa taka kwenye jaa la taka anapoambiwa aitupe.<br>Mwanafunzi anaashiria mpira wa soka anapoulizwa mchezo anaoupenda zaidi. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anajibu ipasavyo kauli rahisi (ikiwemo maelekezo yenye hatua mbili) na maswali.<br>Mwanafunzi anachukua gundi na kushikisha unyoya wake kwenye karatasi, kama alivyoagizwa na mwalimu.<br>Mwanafunzi anamletea rafiki yake sepetu, rafiki yake anaposema kuwa anahitaji kitu cha kuchimba shimo kwenye sehemu ya kuchimba mchanga. | **Mifano/Eleza:** |

## 11. Mwanafunzi anashiriki uzoefu anapoulizwa kufanya hivyo Anazungumza kuhusu fikra, hisia na mawazo yake binafsi.

*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha.

*** Kiashirio hiki kinaungwa mkono na Kiambatisho cha L: Kadi za Rangi zenye Maswali.

Lengo ni mwanafunzi ajibu swali au uzoefu wa sasa na uzoefu wake, huku akizungumza kwa kutumia sentensi nyingi ambazo zinaweza kueleweka na watu wengi.

a. Tumia rundo la kadi za rangi na umpe mwanafunzi achague moja.
b. Kulingana na rangi ambayo mwanafunzi alichagua, utamuuliza maswali kutoka kwa chati.
c. Ikiwa mwanafunzi hakujibu na anaona haya sana, jaribu kumuonyesha mfano na umpe mwanafunzi jibu lako. Jibu lako la swali lilo hilo litakuwa ni gani?
d. Ikiwa mwanafunzi anachukua muda mwingi kujibu akisaidiwa na picha (zaidi ya dakika 3), jaribu kutumia mazingira yaliyo karibu na mwanafunzi. Je, mwanafunzi atazungumza kuhusu vitu vinavyoonekana

| ALAMA | ☐ **Bado** | ☐ **Anaendelea Kujua** | ☐ **Ndiyo** | ☐ **Haitumiki** |
|---|---|---|---|---|
| | Anazungumza/anaonyesha ishara ya sentensi sahili (zenye maneno 1-2). | Anazungumza/anaonyesha ishara ya sentensi sahili (enye maneno 2-3) ambazo zinaweza kueleweka na wale ambao wanafahamu mtindo wa kuzungumza wa mtoto. | Anazungumza/anaonyesha ishara za sentensi za maelezo (maneno 3 - 4 / sentensi 2 -3) ambazo zinaweza kueleweka na watu wengi. | Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi hajibu maswali.<br>Mwanafunzi anachukua dakika 3 kujibu.<br>Mwanafunzi anajibu ndiyo au hapana. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anajibu kwa sentensi fupi.<br>Mwanafunzi anauliza, "Necessito el bano" alipohitaji kuenda msalani.<br>Mwanafunzi anasema, "Nitafanya mimi." | **Mifano**<br>Mwanafunzi anajibu kwa sentensi nyingi.<br>Mwanafunzi alitaja chakula anachokipenda zaidi na ni nani anayekipika vizuri zaidi.<br>Mwanafunzi anazungumza kuhusu kinywaji anachokipenda zaidi na anaomba apewe kinywaji hicho. | **Mifano/Eleza:** |

## 12. Mwanafunzi anazungumza kwa sentensi kamili.

***Wanafunzi wa ELL/DLL wanapaswa kupewa alama ya weledi wao wa Kiingereza kwa kiashirio hiki.

*** Kiashirio hiki kinaungwa mkono na Kiambatisho cha L: Kadi za Rangi zenye Maswali.

Lengo ni mwanafunzi kuzungumza sentensi kwa Kiingereza zenye makosa machache tu.

a. Fanya zoezi sawia na #11. Zungumza Kiingereza tu na uone ikiwa mwanafunzi anazungumza Kiingereza.
b. Ikiwa mwanafunzi alizungumza Kiingereza hapo awali (kabla ya zoezi hili) unaweza kuweka alama ya kiashirio hiki kulingana na maoni yako. Hata hivyo, bila kufanya zoezi, itabidi umpe sentensi sawia kabisa na zile za 2. Nakili ushahidi.

| ALAMA | ☐ **Bado** | ☐ **Anaendelea Kujua** | ☐ **Ndiyo** | ☐ **Haitumiki** |
|---|---|---|---|---|
| | Hawasiliani kwa Kiingereza. | Anawasiliana kwa Kiingereza kwa kutumia neno moja moja, semi fupi fupi alizokariri au sentensi zisizo kamili. | Anawasiliana kwa Kiingereza kwa kutumia sentensi kamili kuhusu mada na dhana mbali mbali bila kufanya makosa mengi ya sarufi. | Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi haelewi Kiingereza.<br>Mwanafunzi hazungumzi Kiingereza. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anajaribu kumuonyesha mtu mzima ndege huko nje. Anaashiria ndege na kupaza sauti akisema "Tazama".<br>Mwanafunzi anaitisha kalamu ya kuchora, kwa kutazama karatasi yake na kusema: "Andika, ninaandika, ninaandika". | **Mifano**<br>Mwanafunzi anasema: “Wikendi hii nitaenda kuona filamu.”<br>Mwanafunzi anapokea zawadi na kujibu: “Asante kwa zawadi hii, Bw. Damaso.” | **Mifano/Eleza:** |

## 13. Mwanafunzi aliandika nambari hadi 20.

*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha.

Lengo ni mwanafunzi kuhesabu kutoka 1 hadi 20, kwa mfululizo unaofaa.

a. Muulize mwanafunzi anaweza kuhesabu hadi nambari gani.
b. Anza kuhesabu pamoja na mwanafunzi (hadi 3) 1, 2, 3, na umuache mwanafunzi aendelee kuhesabu hadi upeo anaoweza kumudu.
c. Nambari ambazo hazisomi vizuri kwa sababu hajafikisha umri au vikwazo vya kuongea zinahesabiwa.
d. Ikiwa mwanafunzi anaweza kuhesabu hadi 20, kwa mfululizo unaofaa, unaweza kunakili taarifa hiyo kama nukuu.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **ALAMA** | ☐ **Bado**<br>Anahesabu hadi 10. | ☐ **Anaendelea Kujua**<br>Anajaribu kuhesabu hadi 20, lakini huenda akaruka nambari, akarudia nambari, au kuweka nambari kwa mfululizo usio sahihi. | ☐ **Ndiyo**<br>Anahesabu hadi 20. | ☐ **Haitumiki**<br>Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Anahesabu hadi 10. | **Mifano**<br>1, 2, 3, 5, 6, 7, 8, 9, 14, 13, 12, 20.<br>Anajaribu kuhesabu hadi 20, lakini huenda akaruka nambari, akarudia nambari, au kuweka nambari kwa mfululizo usio sahihi. | **Mifano**<br>Anahesabu hadi 20. | **Mifano/Eleza:** |

## 14. Mwanafunzi anatambua na kuelezea angalau maumbo 4.

*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha.

*** Kiashirio hiki kinaungwa mkono na Kiambatisho cha M: Kadi za Maumbo - Maumbo ya Jiometri.

Lengo ni mwanafunzi ataje na kueleza angalau maumbo 4.

a. Weka maumbo mbele ya mwanafunzi.
b. Muulize mwanafunzi atambue maumbo yoyote anayoyajua.
c. Ikiwa mwanafunzi anasita (anakawia kwa dakika 1 au anajaribu kufanya jambo lingine) msaidie kwa kumuuliza ikiwa anaona duara? Ikiwa mwanafunzi anaashiria umbo sahihi, basi endelea.
d. Majina ya maumbo ambayo huenda yakasomeka vibaya kwa sababu hajafikisha umri au vikwazo vya kuongea yanahesabiwa.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **ALAMA** | ☐ **Bado**<br>Anatambua maumbo kwa kuyaashiria. | ☐ **Anaendelea Kujua**<br>Anaweza kutambua maumbo 4 kwa kutaja majina yake. | ☐ **Ndiyo**<br>Anataja majina ya maumbo 4 na anaweza kuyaeleza. | ☐ **Haitumiki**<br>Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi anatambua maumbo yasiyozidi 4. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anataja majina ya maumbo 5, 4 kati yao ni sahihi.<br>Mwanafunzi anaashiria na kutaja duara dufu, almasi, duara na *mistatili*. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anaashiria maumbo na kusema hiyo ni pembetatu, duara, hilali, na mraba. Duara ni ya mviringo, pembetatu ina makali, hilali ni ya kijani, na mraba unatoshana. | **Mifano/Eleza:** |

## 15. Mwanafunzi anaeleza mahali vitu vitano vinavyotumika kila siku vipo.

*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha.

*** Kiashirio hiki kinaungwa mkono na Kiambatisho cha N: Vihusishi vya Mahali na Mwendo (ukurasa wa 69).

Lengo ni mwanafunzi kutaja mahali kitu kiko katika hali tano tofauti.

a. Tumia kadi za msamiati wa mahali.
b. Tumia kitu kutoka kwa chumba na urudie kitendo / uigize tena hali hiyo kutoka kwa kadi.
c. Jaribu kumruhusu mwanafunzi aendelee bila usaidizi na uache atumie lugha kuelezea mahali kitu kilipo.
d. Ikiwa mwanafunzi hazungumzi/hajibu, muulize afuate maelekezo yanayotumia maneno ya kuonyesha mahali kitu kilipo. Au kwa kitu kilicho salama na kinachopatikana. Muulize mwanafunzi awekelee kitu juu ya meza, nyuma ya kiti, chini ya kiti, karibu na kiti, na mbele ya kiti.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **ALAMA** | ☐ **Bado**<br>Anafuata maagizo yanayotumia maneno ya kuonyesha mahali kitu kilipo. | ☐ **Anaendelea Kujua**<br>Anatumia msamiati unaofaa kueleza mahali vitu vinne au vichache vilipo (mahali AU utaratibu). | ☐ **Ndiyo**<br>Anatumia msamiati unaofaa kueleza mahali vitu vitano au zaidi vilipo (mahali AU utaratibu). | ☐ **Haitumiki**<br>Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi anaweka kitu juu ya kiti, anapoulizwa kufanya hivyo.<br>Mwanafunzi anaketi kwenye meza ya jikoni anapoelekezwa kufanya hivyo. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anaomba kupewa zamu ya kwanza.<br>Mwanafunzi anatambua ndege juu angani. Mwanafunzi anasema “arriba” (up). | **Mifano**<br>Mwanafunzi anaeleza mahali mpira ulipo kwenye kadi, na jinsi anavyojua. | **Mifano/Eleza:** |

## 16. Mwanafunzi anapanga na kulinganisha vitu 5 kwa kutumia sifa moja.

*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha.

*** Kiashirio hiki kinaungwa mkono na Kiambatisho cha O: Kupanga Vitu kwa kutumia Sifa Moja.

Lengo la mwanafunzi ni kueleza jinsi na ni kwa nini anapanga vitu.

a. Ikiwezekana, jaribu kumuangalia mwanafunzi akicheza na vidude vya kuchezea.
b. Au ujaribu kucheza na mwanafunzi kwa kutumia vitu vilivyo karibu na nyinyi. Penseli, Kalamu za kuchora, Karatasi, Viatu, Viti, Vikombe, n.k.
c. Ni lazima mwanafunzi aweze kueleza ni kwa nini anapanga au kulinganisha vitu tofauti, kwa kutumia (msamiati maalum) sifa kama vile: rangi, ukubwa, uzito, lengo, maumbo, hai dhidi ya visivyo hai, vinavyolika dhidi ya visivyolika n.k.
d. Ikiwa huwezi kumuangalia mwanafunzi au kucheza na yeye, unaweza kutumia karatasi za mazoezi zilizochapishwa tayari - Kiambatisho cha O. Karatasi hizi za mazoezi zikitumika, ni lazima uweke alama ya mwanafunzi kuwa "anaendelea kujua".

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **ALAMA** | ☐ **Bado**<br>Anashughulika na vitendo vya kupima lakini hatumii maneno kueleza sababu zake. | ☐ **Anaendelea Kujua**<br>Anatumia maneno yanayodhihirisha ufahamu wa sifa zinazopimika. | ☐ **Ndiyo**<br>Anapanga hadi vitu 5 akitumia sifa moja na kueleza matokeo. | ☐ **Haitumiki**<br>Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa. |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi anacheza na wanyama na watu.<br>Mwanafunzi anawaweka wanyama wote kwenye upande mmoja wa meza. | **Mifano**<br>Mwanafunzi analinganisha gari dogo na lori. Gari ni dogo, lori ni kubwa.<br>Mwanafunzi anapanga mnyama pamoja na mmea. Mnyama hula mmea.<br>Eleza sifa zinazopimika za vitu kwa kutumia msamiati maalum akitumia karatasi za mazoezi zilizochapishwa tayari. | **Mifano**<br>Linganisha sifa za vitu kwa kutumia msamiati fulani maalum (k.m. Penseli hii ni refu. Hiyo ni fupi.) kwa kuonyesha kwa mikono. | **Mifano/Eleza:** |

## 17. Mwanafunzi anaonyesha kuvutiwa na mada, mawazo, na shughuli mbali mbali.

*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha.

*** Kiashirio hiki huenda kikaripotiwa na familia.

Lengo ni mwanafunzi kuonyesha ari na utayari wa kujifunza mada mpya na kupanua ufahamu wao.

a. Ni lazima mwanafunzi ajitolee na kuonyesha ari ya kusoma, kwa kuvumbua vitu vipya kwa kugusa, kwa kutazama na kuuliza maswali. Familia zitajua ikiwa mwanafunzi ni mdadisi na zinaweza kuripoti kiashirio hiki.

b. Njia nyingine ya kuona ikiwa mwanafunzi anavutiwa ni kuleta kitu fulani kipya. Kitu kipya, au "hazina" mpya na uone ikiwa mwanafunzi anashughulika kiamilifu kujifunza mengi zaidi.

c. Anzisha shughuli zinazohusisha kutumia mikono:
   - a. leta sepetu - ili kuchimba mchanga na kupanda mbegu zako mwenyewe
   - b. leta maelezo ya mapishi - ili kutengeneza aiskrimu au pudini
   - c. leta kitu ambacho kimegandizwa kwa barafu (maua, majani, n.k.) - ili mwanafunzi afikirie jinsi atayeyusha barafu.




| ALAMA | ☐ **Bado** | ☐ **Anaendelea Kujua** | ☐ **Ndiyo** | ☐ **Haitumiki** |
|---|---|---|---|---|
| | Anaonyesha kuvutiwa na mazingira yake. | Anaonyesha kuvutiwa na mada, kitu, au uzoefu fulani. | Anaonyesha kuvutiwa na uzoefu mpya kwa kuwatazama wengine, kushika vitu, au kuuliza maswali. | Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa. |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi anakagua vitu kwa kuvigusa. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anaonyesha kuvutiwa na anatangamana na wengine kuhusu kazi na vitendo vyao. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anauliza maswali ili kuelewa jambo.<br>Mwanafunzi anauliza: “Hiki hufanya nini?” | **Mifano/Eleza:** |

## 18. Mwanafunzi anashiriki kufanya shughuli moja kwa muda mrefu.

*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha.

*** Kiashirio hiki huenda kikaripotiwa na familia.

Lengo ni mwanafunzi ashiriki kikamilifu katika shughuli kwa zaidi ya dakika 15.

a. Unaweza kumuuliza mzazi atoe maoni yake na uandike mfano.

b. Mwanafunzi anashiriki katika shughuli ambayo amejichagulia, hajajichagulia, au shughuli ambayo hapa awali ilikuwa ni tatizo.

c. Ni lazima mwanafunzi ashiriki kwa kipindi kirefu, bila kuvutwa mawazo, kutovutiwa tena, na bila kuhimizwa na mtu mzima.

d. Skrini – Muda: Kutazama televisheni au kucheza mchezo kwenye kompyuta hakuhesabiwi.

e. Muda mrefu unachukuliwa kuwa zaidi ya dakika 15.

| ALAMA | ☐ **Bado** | ☐ **Anaendelea Kujua** | ☐ **Ndiyo** | ☐ **Haitumiki** |
|---|---|---|---|---|
| | Anashiriki kwa shughuli lakini anavutwa mawazo | Anashiriki kwa shughuli lakini anavutwa mawazo au kupoteza mvuto asipohimizwa na mtu mzima. | Anaendelea na shughuli hata kwenye mazingira yanayomvuta mawazo au wakati<br>jambo linapokuwa gumu. | Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa. |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi anacheza na treni, baada ya dakika 5 mwanafunzi anataka kutoka nje. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anachora picha ya jamaa, baada ya dakika 10 mwanafunzi anasema: "Nimemaliza". Mtu mzima anamuhimiza kuongezea rangi zaidi. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anatengeneza mashua kwa kutumia nyenzo ya kufinyaga; mashua inaendelea kuzama. Mwanafunzi hakati tamaa, hata wanafunzi wale wengine wakitengeneza mashua zinazoelea. | **Mifano/Eleza:** |

## 19. Mwanafunzi anatumia nyenzo na vitu kuwakilisha dhana mpya.

*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha.

*** Kiashirio hiki huenda kikaripotiwa na familia.

Lengo la mwanafunzi ni kutumia fikra na ubunifu wake.

a. Ni lazima mwanafunzi aonyeshe kuwa anaweza kucheza na vitu tofauti na ni mbunifu katika mchezo wake.
b. Chombo kinachotumiwa hakiwezi kufanana (kufanya kazi) na kile wanachocheza nacho.
c. Mchezo wa kujifanya ni lazima uwakilishe dhana mpya, maana nje ya maisha ya kila siku, fikra, nje ya mila za utamaduni wake.
d. Je, mwanafunzi ana mawazo pevu na yenye ubunifu?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **ALAMA** | ☐ **Bado**<br>Anatumia vitu halisi kucheza na kubuni. | ☐ **Anaendelea Kujua**<br>Anatumia vitu halisi kuwakilisha dhana kuu. | ☐ **Ndiyo**<br>Anatumia vitu tofauti kuwakilisha kitu kipya, huku akikipa utendaji na mwendo. | ☐ **Haitumiki**<br>Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa. |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi anatumia ndege ya kuchezea kupaa kwenye chumba. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anatumia kalamu ya kupakia rangi ili kupiga mswaki meno ya mwanasesere na kuchana nywele zake.<br>Mwanafunzi anatumia karatasi kutengeneza fimbo yake ya kuchezea. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anatumia vyungu vya jikoni kutengeneza ngoma na kujifanya kucheza kwenye bendi mpya ya muziki wa Kitamaduni (Country). | **Mifano/Eleza:** |

## 20. Mwanafunzi anajaribu kukamilisha zoezi kwa zaidi ya njia moja, kabla ya kuomba usaidizi au kuacha anaposhindwa.

*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha.

*** Kiashirio hiki kinaungwa mkono na Kiambatisho cha P: Usuluhishaji wa Tatizo.

Lengo la mwanafunzi ni kuweza kusema mawazo/suluhu zake ili kutatua matatizo kadhaa.

a. Simulia hadithi ya kijamii - mwambie mwanafunzi atoe suluhu tofauti za tatizo linalowasilishwa kwenye hadithi.
b. Mpira unakwama kwenye mti - tumia mpira wa tenisi / mpira wa soka - Unafikiri tunawezaje kuufikia mpira huo?
c. Sahau kuhusu ufunguo wa kuingia ndani ya nyumba - Unafikiri mtoto anaweza kuingia vipi ndani ya nyumba?
d. Watoto wawili wanapigania lori moja - Unafikiri tunawezaje kuwakomesha wasipigane?
e. Mtoto anataka tufaa lililo mtini - Unafikiri mtoto anawezaje kufikia tufaa hilo?
f. Fumbo

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **ALAMA** | ☐ **Bado**<br>Anaonyesha kutobadilisha fikra anapojaribu kutatua tatizo. | ☐ **Anaendelea Kujua**<br>Anajaribu kutatua matatizo rahisi kwa kubahatisha AU kuiga mkakati uliotumiwa na mtu mzima au mwenzake. | ☐ **Ndiyo**<br>Anajaribu kutatua matatizo kwa kutumia zaidi ya mbinu moja, na kutambua anapohitaji usaidizi. | ☐ **Haitumiki**<br>Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa. |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi anatumia mkakati mmoja tu kusuluhisha tatizo lililo kwenye picha/hadithi.<br>Mwanafunzi anarudia kosa mara nyingi. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anatumia mbinu ya kubahatisha ili kutatua fumbo.<br>Mwanafunzi ana mawazo ya kutatua matatizo yaliyo kwenye picha/hadithi, lakini sio mawazo yote yanafaulu. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anaitisha usaidizi ili kukamilisha zoezi kwa pamoja.<br>Mwanafunzi anatoa suluhu nyingi tofauti za tatizo lililo kwenye picha/hadithi. | **Mifano/Eleza:** |

## 21. Mwanafunzi anatambua na kuonyeshana sehemu za mwili.

*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha.

*** Kiashirio hiki kinaungwa mkono na Kiambatisho cha Q: Sehemu za Mwili.

Lengo ni mwanafunzi kuashiria na kutaja majina ya sehemu kadhaa za mwili.

a. Sehemu ya kwanza ya Kiambatisho cha Q ni kufanya mazoezi ya kuonyesha na kutambua majina ya sehemu za mwili.
b. Sehemu ya pili ya Kiambatisho ni michoro ya mvulana na msichana. Ambapo mwanafunzi anaweza kuashiria (au kupaka rangi/kuweka alama) na kutaja jina la kila sehemu ya mwili.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **ALAMA** | ☐ **Bado** Anaonyeshana baadhi ya sehemu za mwili. | ☐ **Anaendelea Kujua** Anatambua baadhi ya sehemu za mwili. | ☐ **Ndiyo** Anatambua na kuonyeshana sehemu kadhaa za mwili. | ☐ **Haitumiki** Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa |
| **MADOKEZO** | **Mifano** Mwanafunzi anaweza kuashiria sehemu kadhaa za mwili ambazo ameulizwa. | **Mifano** Mwanafunzi anaweza kutaja majina ya sehemu kadhaa za mwili ambazo unaashiria pia. | **Mifano** Mwanafunzi anaweza kutambua na kuonyeshana sehemu kadhaa (angalau 10) za mwili bila usaidizi wowote. | **Mifano/Eleza:** |

## 22. Mwanafunzi anatambua na kuonyesha desturi muhimu za afya njema.

*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha.

*** Kiashirio hiki huenda kikaripotiwa na familia.

Lengo la mwanafunzi ni kuweza kutambua na kufanya desturi bora za afya na usafi wa kimsingi peke yeke.

a. Mwanafunzi anapaswa kuwa anaweza kunawa mikono kwa sekunde 20.
b. Mwanafunzi amefunzwa kikamilifu jinsi ya kutumia choo.
c. Mwanafunzi anapaswa kufuata desturi ya matumizi ya choo - kuenda msalani - kunawa mikono baadaye.
d. Mwanafunzi anapiga meno yake mswaki bila usaidizi.
e. Mwanafunzi anaweza kujivalisha nguo.
f. Mwanafunzi anaelewa kile anachopaswa kuvaa mchana na usiku.
g. Mwanafunzi ana utaratibu maalum wa wakati wa kulala - na anapumzika vya kutosha kwa ajili ya "siku ya shule" inayofuata.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **ALAMA** | ☐ **Bado** Mwanafunzi hafahamu desturi za kimsingi za afya. | ☐ **Anaendelea Kujua** Anafanya desturi za kimsingi anapokumbushwa na mtu mzima. | ☐ **Ndiyo** Anafanya desturi za kimsingi bila usaidizi. | ☐ **Haitumiki** Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa. |
| **MADOKEZO** | **Mifano** Mwanafunzi hajui jinsi ya kupiga meno yake mswaki, au ni wakati gani anafaa kunawa mikono.<br>Mwanafunzi hana ratiba au utaratibu.<br>Mwanafunzi hawezi kujivalisha nguo bila usaidizi. | **Mifano** Mwanafunzi anafahamu jinsi ya kufanya taratibu za kimsingi, lakini anahitaji kukumbushwa na mtu mzima kuzifanya.<br>Mwanafunzi anafahamu taratibu 3 kati ya 5. | **Mifano** Mwanafunzi anafahamu na anafanya angalau taratibu 5 za kimsingi bila usaidizi. | **Mifano/Eleza:** |

## 23. Mwanafunzi anakula na kunywa akitumia vifaa vinavyofaa bila kusaidiwa.

*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha.

*** Kiashirio hiki huenda kikaripotiwa na familia.

Lengo ni mwanafunzi kujitegemea na kuweza kutumia vyombo vyote anavyopewa shuleni kwa njia inayofaa.

a. Je, mwanafunzi wako anaweza kula akitumia vyombo vinavyofaa? (Uma, kijiko, kisu)
b. Je, mwanafunzi wako anaweza kujitilia kinywaji chake na kunywa akitumia vyombo vinavyofaa, bila kukimwaga? (Kikombe)
c. Je, mwanafunzi wako anaweza kubeba trei yenye sahani, kitambaa cha mezani na vyombo vyote?

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **ALAMA** | ☐ **Bado**<br>Anaonyesha ufahamu wa kimsingi wa vyombo. | ☐ **Anaendelea Kujua**<br>Anatumia vyombo akimwaga kidogo. | ☐ **Ndiyo**<br>Anatumia vyombo vyote ipasavyo, bila kumwaga. | ☐ **Haitumiki**<br>Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa. |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi anafahamu matumizi ya kila chombo, lakini hawezi kuvitumia bila kusaidiwa. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anaweza kula na kunywa kwa kutumia mikono yake bila kusaidiwa.<br>Mwanafunzi anamwaga chakula au kinywaji wakati mwingine. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anakula na kunywa bila kusaidiwa.<br>Mwanafunzi anatumia vyombo vyote kwa njia inayofaa. | **Mifano/Eleza:** |

## 24. Mwanafunzi anatumia misuli yake kusonga sana anapotumia kifaa.

*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha.

*** Kiashirio hiki huenda kikaripotiwa na familia.

Lengo ni mwanafunzi kuweza kusongeza misuli yake sana kwa wakati mmoja.

a. Ikiwa hauna mpira au kamba yoyote. Tengeneza mpira wako kwa kutumia karatasi na kuikunja kuwa umbo la mviringo.
b. Mwambie mwanafunzi atupe mpira huku akitembea au kukimbia.
c. Mwambie mwanafunzi aruke. Weka karatasi sakafuni. Mwambie mwanafunzi airuke kwa kutumia miguu miwili: kutoka kushoto hadi kulia, kutoka mbele hadi nyuma. Mwambie mwanafunzi arudie kuruka vivyo hivyo lakini akiwa ametenganisha miguu. Ili miguu yote miwili iwe kwenye pande tofauti za karatasi.
d. Mwambie mwanafunzi apande na kushuka kwenye vipandio. Au kipandio kimoja mara nyingi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **ALAMA** | ☐ **Bado**<br>Anasonga kwa uratibu unaoongezeka. | ☐ **Anaendelea Kujua**<br>Anafanya mienendo midogo kwa kujiamini na kwa urahisi. | ☐ **Ndiyo**<br>Ana ujuzi wa kufanya mienendo mikubwa kwa kujiamini na kwa urahisi. | ☐ **Haitumiki**<br>Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi anajaribu kuruka.<br>Mwanafunzi anajaribu kupiga mpira kwa mguu. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anasonga na kusimama kwa udhibiti..<br>Mwanafunzi anajaribu kuhesabu huku akiruka.<br>Mwanafunzi anapiga mpira kwa mguu au kuurusha. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anakimbia na kuupiga mpira.<br>Mwanafunzi anapanda na kushuka kwenye vipandio akibadilisha nyayo bila kujishikilia kwenye nguzo au ukuta. | **Mifano/Eleza:** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **25. Mwanafunzi anafunga zipu, vifungo, anajifunga na kujifungua nguo za nje.**<br>*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha.<br>*** Kiashirio hiki huenda kikaripotiwa na familia. | | | | |
| Lengo ni mwanafunzi kuweza kujivalisha na kujivua nguo.<br>a. Mwanafunzi anaweza kufunga na kufungua zipu.<br>b. Mwanafunzi anaweza kufunga vifungo vya shati au jaketi (koti).<br>c. Mwanafunzi anaweza kufungua vifungo vya shati au jaketi (koti).<br>d. Mwanafunzi anaweza kuvaa viatu na suruali zinazofungwa kwa kishikizo cha kubandika.<br>e. Mwanafunzi anaweza kufunga kamba za viatu vyake.<br>f. Mwanafunzi anaweza kuvaa/kuvua jaketi yake.<br>g. Mwanafunzi anaweza kuvaa/kuvua viatu vyake.<br>h. Mwanafunzi anaweza kuvaa/kuvua soksi zake.<br>i. Mwanafunzi anaweza kuvaa/kuvua suruali yake.<br>j. Mwanafunzi anaweza kuvaa/kuvua glovu zake. | | | | |
| **ALAMA** | ☐ **Bado**<br>Hawezi kufanya mazoezi haya ya kusongeza misuli. | ☐ **Anaendelea Kujua**<br>Anajaribu kufanya mazoezi haya ya ustadi wa kusongeza misuli, akisaidiwa na mtu mzima. | ☐ **Ndiyo**<br>Anajizoesha kusongeza misuli bila usaidizi. | ☐ **Haitumiki**<br>Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi anaudhika na anahitaji usaidizi kuvaa au kuvua nguo. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anaweza kufungua zipu ya jaketi yake na anaomba usaidizi ili kuvaa jaketi yake. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anaweza kujivalisha nguo.<br>Je, mtoto wako anaweza kujivua nguo za nje (koti, buti, kofia, kinga za mikono) (ikiwemo kufunga zipu, kufungua vifungo, na kufunga)? | **Mifano/Eleza:** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **26. Mwanafunzi anatumia makasi kwa kujidhibiti na akiwa na dhamira.**<br>*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia katika lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha.<br>*** Kiashirio hiki kinaungwa mkono na Kiambatisho cha R: Ujuzi wa Kutumia Makasi. | | | | |
| Lengo ni mwanafunzi aweze kushika makasi ipasavyo na awe anaweza kukata mstari uliojipinda na mstari ulionyooka.<br>a. Tumia karatasi za mazoezi ili kujizoesha.<br>b. Mwanafunzi atatumia karatasi za mazoezi ambazo zina mistari.<br>c. Ili mwalimu aamue kiwango cha ujuzi, ni lazima mwanafunzu akate **<u>kwenye mstari</u>**. | | | | |
| **ALAMA** | ☐ **Bado**<br>Haonyeshi kujidhibiti anapotumia makasi. | ☐ **Anaendelea Kujua**<br>Anatumia makasi kwa kujidhibiti ili kukata karatasi. | ☐ **Ndiyo**<br>Anatumia makasi kwa kujidhibiti na akiwa na dhamira ili kukata karatasi ya mazoezi aliyopewa. | ☐ **Haitumiki**<br>Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br>Mwanafunzi anashika makasi yakiwa mbali, jambo linalofanya asiweze kukata karatasi.<br>Mwanafunzi hawezi kukata karatasi. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anashika makasi vizuri na anaweza kukata mistari kadhaa. | **Mifano**<br>Mwanafunzi anakata mstari ulionyooka, na anakata mstari uliojipinda. | **Mifano/Eleza:** |

## ✧ 27. Mwanafunzi anaandika na kuchora akiwa ameishikilia ipasavyo.

*** Wanafunzi wa ELL/DLL wanaweza kudhihirisha dalili za tabia kwa lugha yao kuu, au kupitia mikakati isiyohusisha lugha

Lengo ni mwanafunzi kuonyesha kuwa anaweza kushika kalamu kwa njia inayofaa na kuidhibiti anapoisongesha.

a. Angalia kiashirio hiki kila wakati mwanafunzi anashika kalamu ya kuandika, kalamu ya kuchora au penseli.
b. Ikiwa hauna uhakika na kiwango cha ujuzi cha mwanafunzi, mwambie mwanafunzi aandike jina lake kwenye karatasi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **ALAMA** | ☐ **Bado**<br>Anashikilia kwa nguvu kwa udhibiti mdogo wa jinsi anavyoisongesha. | ☐ **Anaendelea Kujua**<br>Anashikilia ipasavyo lakini ana udhibiti mdogo wa jinsi anavyoisongesha. | ☐ **Ndiyo**<br>Anaishikilia ipasavyo (kati ya kidole gumba na kidole cha shahada) na anadhibiti vizuri jinsi anavyoisongesha. | ☐ **Haitumiki**<br>Kiwango cha ujuzi hakiwezi kutambuliwa |
| **MADOKEZO** | **Mifano**<br><br>Mwanafunzi anashika kifaa cha kuandika kwa ngumi yake.<br>Mwanafunzi anachora kwa kutumia ujuzi wa kusongesha misuli mikubwa (bega). | **Mifano**<br><br>Mwanafunzi anashika kifaa cha kuandika kwa kiganja chake.<br>Mwanafunzi anatumia mkono, kiwiko kikiwa kimeelekea nje, kuchora. | **Mifano**<br><br>Mwanafunzi anatumia vidole vitano, vinne au vitatu ili kushika kifaa chake cha kuchora.<br>Mwanafunzi anachora kwa kusongesha kifundo cha mkono.<br> | **Mifano/Eleza:** |